



Bima ya Child Health Plus kwa Kifupi

NI NANI ANAYESTAHIKI?

WATOTO AMBAO:

- Wa umri wa chini ya miaka 19
- Ni wakazi wa Jimbo la New York
- Hawastahiki kupokea bima ya Medicaid
- Hawamo katika bima nyingine ya afya
- Hawastahiki au hawajasajiliwa katika bima ya afya kupitia mpango wa huduma ya afya ya jimbo (NYSHIP)
- Watoto wanaweza kustahiki bila kuzingatia hali yao ya uhamiaji

NY State of Health inazingatia sheria za haki za raia za Shirikisho zinazotumika na haibagui kwa msingi wa mbari, rangi, asili ya taifa, dini, jinsi, umri, hali ya ndoa/familia, rekodi za kukamatwa, hukumu za uhalifu, utambulisho wa jinsia, mwelekeo wa kingono, sifa za kinasaba, hali ya jeshi, hali ya mhanga wa unyanasaji wa nyumbani, na/au kulipiza kisasi.

NINI KINACHOJUMUISHWA?

- Mahudhurio ya kupimwa
- Uchunguzi wa kimwili
- Chanjo
- Huduma za maabara na pichatiba
- Huduma za dharura
- Dawa za kuagizwa na daktari
- Dawa zisizo za kuagizwa na daktari, ikiwa utaruhusiwa na daktari
- Huduma ya wagonjwa wanaolazwa
- Huduma za wagonjwa wasiolala za tiba za muda mfupi (tibakemo, usafishaji wa damu)
- Huduma za afya ya kiakili na ugonjwa wa matumizi ya madawa ya kulevya kwa wagonjwa wanaolazwa na wasiolazwa
- Huduma za Meno na Macho
- Huduma za Kuongea na Kusikia
- Vifaa vya Matibabu Vinavyodumu
- Kituo cha Kutunza Wagonjwa

WASILIANA NASI:

nystateofhealth.ny.gov | 1-855-355-5777 au TTY 1-800-662-1220

GHARAMA YA MPANGO WA CHILD HEALTH PLUS NI GANI?

MALIPO YA KILA MWEZI: Bei ya kila mwezi hutegemeana na pato la familia na ukubwa wa familia.* Hakuna malipo ya juu ya kila mwezi kwa familia zenye mapato ya chini. Familia zenye mapato ya juu hulipa malipo ya juu ya kila mwezi, kulingana na jedwali hapa chini. Kwa familia kubwa zaidi, kiwango cha juu zaidi cha ada ya kila mwezi ni cha watoto watatu tu. Familia zenye mapato ya kiasi cha juu ya kilichojumuishwa kwenye bima wanaweza kulipa kiasi chote, kinachotofautiana kulingana na mpango mahsusi wa afya.

KUGAWANA GHARAMA: Mpango wa Child Health Plus hauna ada za kila mwaka zinazokatwa wala malipo saidizi.

Kiasi cha Juu Zaidi cha Mapato ya Kila Mwaka Kulingana na Ukubwa wa Familia				Mchango wa Kila Mwezi kwa Kila Mtoto (idadi ya juu zaidi ya watoto unaolipia ni 3)
1	2	3	4	
chini ya \$19,984	chini ya \$27,056	chini ya \$34,128	chini ya \$41,200	0
\$27,728	\$37,541	\$47,353	\$57,165	\$9 (kiasi cha juu zaidi cha \$27)
\$31,225	\$42,275	\$53,325	\$64,375	\$15 (kiasi cha juu zaidi cha \$45)
\$37,470	\$50,730	\$63,990	\$77,250	\$30 (kiasi cha juu zaidi cha \$90)
\$43,715	\$59,185	\$74,655	\$90,125	\$45 (kiasi cha juu zaidi cha \$135)
\$49,960	\$67,640	\$85,320	\$103,000	\$60 (kiasi cha juu zaidi cha \$180)
zaidi ya \$49,960	zaidi ya \$67,640	zaidi ya \$85,320	zaidi ya \$103,000	Malipo kamili, hutegemea mpango wa afya

*Kulingana na Viwango vya Mali vya Shirikisho (FPL) 2019 Viwango vya mapato vinaweza kurekebishwa kila mwaka kulingana na mabadiliko ya FPL.